



# Andiswa Nyota wa Mpira wa Miguu

- Eden Daniels
- Eden Daniels
- Matteo E. Mwita
- 2
- Kiswahili SW



Andiswa alikuwa anawaangalia wavulana wakicheza mpira wa miguu. Alitamani kujiunga nao. Akamwomba kocha kufanya nao mazoezi.



Kocha akaweka mikono kiunoni. "Kwenye shule hii, ni wavulana pekee wanaoruhusiwa kucheza mpira wa miguu," alisema.



Wavulana walimwambia aende kucheza mpira wa wavu. Walisema mpira wa wavu ni kwa ajili ya wasichana na mpira wa miguu ni kwa wavulana. Andiswa alijisikia vibaya.



Siku iliyofuata, shule yao ilikuwa na mashindano makubwa ya mpira wa miguu. Kocha alikuwa na wasiwasi kwa kuwa mchezaji wake wa kutegemewa alikuwa mgonjwa na asingecheza.



Andiswa alimwendea kocha na kumuomba kumruhusuacheze. Kocha hakujua afanye nini. Akaamua kumruhusu Andiswe ajiunge na timu.



Mchezo ulikuwa mgumu. Hakuna timu yoyote iliyokuwa imefunga goli hadi muda wa mapumziko.



Wakati wa kipindi cha pili kijana mmoja alimpatia Andiswa mpira. Akakimbia kwa kasi sana kuelekea golini. Akaupiga mpira kwa nguvu na akafunga goli.



Umati ukashangilia kwa vifijo na furaha.  
Kuanzia siku hiyo, wasichana waliruhusiwa  
kucheza mpira wa miguu kwenye timu ya  
shule.



# Global Storybooks

[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)

## Andiswa Nyota wa Mpira wa Miguu

Eden Daniels

Eden Daniels

Matteo E. Mwita

